





TaTEDO-SESO ni taasisi ya kiraia ya kuendeleza huduma za nishati endelevu yenye uzoefu wa zaidi ya miaka 30. Lengo mahususi la taasisi ni kuboresha maisha ya jamii kwa kuongeza upatikanaji wa huduma za nishati endelevu kwa wote.

Jumuiko la Maliasili Tanzania — Tanzania Natural Resource Forum

Jumuiko la maliasili Tanzania ni asasi ya kiraia iliyosajiliwa Tanzania mwaka 2006 yenye lengo la kuboresha utawala na uwajibikaji katika usimamizi wa maliasili hususani ardhi, maeneo ya malisho, misitu, na wanyamapori, Pamoja na kufanya tafiti mbalimbali.


P.O. Box 32794 Dar es salaam

tatedotz | energy@tatedo.or.tz | www.tatedo.or.tz

tatedo | tatedoenergy | +255 738 201 498





Co-funded by the European Union


# MRADI JUMUISHI WA KUHIFADHI MISITU

## NA KUBORESHA MNYORORO WA THAMANI WA MKAA

Kujengea uwezo jamii kwenye maswala ya mnyororo wa thamani wa mkaa na usimamizi endelevu wa kuhifadhi misitu pamoja na kuboresha maisha katika jamii..

### Watekelezaji wa Mradi

TaTEDO - SESO

Jumuiko la Maliasili Tanzania — Tanzania Natural Resource Forum

## UTANGULIZI

Mkaa ni moja ya chanzo cha mapato cha wananchi wa Mkoa wa Pwani, pia ni moja ya nishati kuu inayotumika kupikia katika mkoa wa Dar es Salaam. Sehemu kubwa ya mkaa huvunwa kutoka kwenye misitu ya asili ikiwemo misitu ya vijiji. Kwa kiwango kikubwa uvunaji wa miti, uchomaji mkaa na biashara hufanyika pasipo kufuata taratibu na miongozo iliyowekwa na mamlaka husika na hivyo kuchangia uharibifu wa misitu.

**Mradi Jumuishi wa Kuhifadhi Misitu na kuboresha Mnyororo wa Thamani wa Mkaa (ISU-CHAVPRO)** unakusudia kujengea jamii uwezo wa kutunza na kusimamia misitu na mnyororo wa thamani wa mkaa kwa maendeleo ya jamii na kiuchumi. Mradi huu ni wa miaka mitatu ambao ulianza Oktoba 2023 na unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kusimamiwa na Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi unatekelezwa katika wilaya tano za mkoa wa Pwani ambazo ni Rufiji, Kibiti, Mkuranga, Kisarawe na Bagamoyo.

Watekelezaji wa mradi ni Taasisi ya huduma ya Nishati Endelevu (TaTEDO-SESO) kwa ushirikiano na Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF) pamoja na Halmashauri za Wilaya katika maeneo husika.

## DHUMUNI LA MRADI

Kuboresha uwezo wa jamii katika wilaya tano za Mkoa wa Pwani kwa kuhifadhi misitu na kuongeza tija kwenye mnyororo wa thamani wa mkaa kwa ustawi wa jamii na kutunza mazingira.

## KAZI MUHIMU ZA MRADI

- Kuwezesha uandaaji na usimamizi wa mipango ya matumizi bora ya ardhi.
- Kuongeza uelewa wa jamii katika kutekeleza sera, mikakati miongozo, sheria zinazosimamia misitu na mnyororo wa thamani wa mkaa.
- Kuwezesha uandaaji wa mipango ya usimamizi wa misitu ya vijiji na kuimarisha kamati za usimamizi.
- Kupunguza utegemezi wa misitu ya asili katika uzalishaji wa mkaa kupitia uanzishaji wa mashamba ya miti, kilimo mseto na kuwezesha uzalishaji wa mkaa mbadala.
- Kujenga uwezo kwa wachoma mkaa katika kutumia njia endelevu za uvunaji na uchomaji mkaa ikiwemo tanuri lililoboreshwa.
- Kuwezesha uanzishwaji wa umoja wa wazalishaji, wasafirishaji na wafanyabiashara wa mkaa ili kuimarisha usimamizi.
- Kuanzisha vyanzo mbadala vya kipato ambavyo ni rafiki katika usimamizi na utunzaji misitu.
- Kuchagiza usawa wa kinjisia na makundi maalumu.



## MATOKEO TARAJIWA YA MRADI

Mradi utachangia kupunguza kasi ya ukataji miti, kupunguza uharibifu wa misitu, kutoweka kwa bioanuwai. Pia utachangia kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi. Utaongeza ajira na upatikanaji wa nishati safi. Kupitia utekelezaji wa mradi, ushirikiano kati ya wadau mbalimbali wanaohusika na misitu na mazao yake utaimarika.